International Community of Women Living with HIV Eastern Africa (ICWEA)

MUHTASARI WA UTAFITI KWA WATUNGAJI SERA

# Kusaidiwa Kujulisha Mchumba Kwamba Una Ukimwi

## *Uwezekano wa Kusababisha Uhasama na Athari Zake kwa Wanawake na Wasichana*



# Muktadha wa sera:

Kusaidiwa kujulisha mchumba umekuwa mkabala muhimu unaotumiwa na maafisa wa afya katika kutibu magonjwa yanayosambazwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine kwa miongo kadha, mkiwemo mipango inayolenga magonjwa ya zinaa na kifua kikuu (TB). Mikabala ya kuwajulisha wachumba hali yao ya afya imeonekana kuwa inafaulu katika kupima na kutibu magonjwa ya zinaa na kuzuia kuambukizwa tena. Vile vile, kuendelea kufuatilia watu wenye uhusiano na wagonjwa na vipimo vya kujitolea kwa jamaa za wagonjwa wa TB ni njia bora na iliyo mwafaka ambayo imetumika na ikafaulu kwenye jumuiya zenye kiasi kikubwa cha wagonjwa wa Ukimwi na TB. Kufikia mwisho wa mwaka 2015, ilikadiriwa kwamba zaidi ya watu miliyoni 36 duniani kote walikuwa na Ukimwi, na asilimia 40 kutoka idadi hiyo walikuwa hawajapimwa. Ili kuziba pengo hili na kutimiza malengo ya vipimo na matibabu ya shirika la UNAIDS (malengo ya 90:90:90), mikakati mipya ilihitajika ili kuwezesha vipimo vingi sana na vyenye kiwago bora. Mkakati kusaidiwa kujulisha mchumba unaweza kusababisha ongezeko la vipimo wakati pia watu wenye Ukimwi ambao hawajapimwa watajulikana.

**Kujulisha mchumba au kufualitia watu wenye uhusiano na mgonjwa** kunafasiliwa kuwa mchakato wa kujitolea ambapo afisa mshauri anawauliza watu ambao wamepimwa na kugunduliwa wa Ukimwi kutoa taarifa kuhusu wachumba zao wanaoshiriki ngono nao na/au wanaotumia pamoja madawa ya kujidunga sindano. Mara tu habari hizi zikipatikana na hao watu waliogunduliwa kuwa na Ukimwi wakatoa ruhusa, wahusika wao wanapewa huduma za kupimwa Ukimwi. Kujulisha mchumba kunafanyika kupitia ama njia ya kibinafsi au njia ya kusaidiana. **Huduma za kujulisha mchumba kibinafsi** ni pamoja na afisa mshauri kuwahimiza wagonjwa wa Ukimwi kuwajulisha wachumba wao wa kingono au wa kujidunga madawa kwamba waligunduliwa kuwa na Ukimwi na kisha kuwapendekezea waende wakapimwe Ukimwi pia kwa vile wamehatarishwa kuambukizwa Ukimwi. **Huduma za kusaidiwa kujulisha mchumba hali ya Ukimwi** inazingatia kuwasaidia wagonjwa wa Ukimwi waliotoa idhini na afisa mshauri kutangaza hali yao ya kuwa wagonjwa au kuwajulisha wachumba kisiri kwamba huenda wakawa wameambukizwa Ukimwi. Afisa wa afya pia hujitolea kuwapima Ukimwi hao wachumba. Mpango huu hufanyika kwa kupitia mikabala ya rufaa ya kimkataba, rufaa ya afisa wa afya au rufaa ya ubia. Rufaa ya kimkataba hufanyika pale wagonjwa wa Ukimwi wanapofanya mkataba wa rasmi na huyu afisa wa afya na kukubali kwamba wao wenyewe watatjulisha wachumba wao kwamba wana ugonjwa wa Ukimwi na kisha kuelekeza wachumba wao kupata huduma za kupimwa Ukimwi ndani ya muda fulani uliokubaliwa na huyu mgonjwa wa Ukimwi. Iwapo mchumba wa mgonjwa wa Ukimwi hawezi kupata huduma za kupimwa Ukimwi au kuwasiliana na kituo cha afya kinachohusika ndani ya muda huo, afisa wa afya atamfikia mchumba huyu moja kwa moja na kujitolea kumpima Ukimwi. **Rufaa ya afisa wa afya** hufanyika pale mgonjwa wa Ukimwi anapokubali kwamba afisa mshauri awasiliane kisiri na mchumba au wachumba wa mgonjwa huyu na kujitolea kuwapima Ukimwi. **Rufaa ya ubia** hufanyika pale afisa mshauri anaandamana na wagonjwa wa Ukimwi kuwawezesha kujulisha wachumba wao kwamba wana ugonjwa wa Ukimwi na kwamba wachumba wao huenda wakawa wameambukizwa Ukimwi pia. Afisa wa afya pia hujitolea kuwapima Ukimwi wachumba hao. Lakini, kumekuwa na malalamiko kwamba mkakati wa mtu kusaidiwa kujulisha mchumba akigunduliwa kuwa na Ukimwi unaweza


kusababisha uhasama dhidi ya mtu huyu aliyetangaza kuwa ana Ukimwi, uhasama huo ukiwa madhara ya kimwili, kingono, au kimawazo kutoka kwa mchumba wake wa sasa au wa awali. Uhasama huu unaweza kutokea kati ya wachumba wa jinsia moja au jinsia tofauti. Kuna wakati ambapo mkakati huu umesababisha madhara mengine ya kijamii, kwa mfano, talaka au kuzoroteka kwa uhusiano wa kimapenzi. Katika ngazi ya dunia, kwa mujibu wa chapisho la idara ya Umoja wa Mataifa ya mambo ya wanawake[1] na jinsia la mwaka 2016, ilikadiriwa kwamba kulikuwa na takribani wanawake miliyoni 18 wenye umri wa miaka 15 kwenda juu ambao wana Ukimwi, ambao ni mgao wa asilimia 52 ya watu wazima wote wenye Ukimwi. Wasichana wenye umri kati ya miaka 15-24 ndio wameathirika zaidi. Pia, takribani wasichana miliyoni mbili na nusu walikuwa na ugonjwa wa Ukimwi, ambao ni mgao wa asilimia 61 wa vijana wote wenye Ukimwi (wenye umri kati ya miaka 15-24). Kuna hitilafu za kieneo katika idadi ya wanawake wapya walioambukizwa Ukimwi na katika mgao wa wanawake wenye Ukimwi (wenye umri wa miaka 15 kwenda juu) ikilinganishwa na idadi ya wanaume; na hitilafu hizi ziko bayana zaidi miongoni mwa vijana wasichana (wenye umri wa miaka kati ya 15-24) ikilinganishwa na vijana wavulana. Katika nchi za kusini ya Sahara, wanawake wanachukua mgao wa asilimia 56 ya maambukizi mapya ya Ukimwi kwa watu wazima (miaka 15 kwenda juu); na idadi ilikuwa juu zaidi miongoni mwa vijana wa kike wenye umri wa miaka kati ya 15-24 wakichukua mgao wa asilimia 67 ya vijana wote wapya walioambukizwa Ukimwi. Hitilafu hii katika maambukizi ya Ukimwi miongoni mwa wanawake huwafanya kuwa hatarini kufikwa na uhasama kutoka kwa wachumba wao kwani wakati mwingi wao ndio wa kwanza kupimwa Ukimwi.

1 UN Women (July 2018) Facts and figures: HIV and AIDS



## Mazingira ya Utungaji Sera

Katika mwaka wa 2016, Shirika la Afya la Dunia liliunda miongozo ya kuwezesha huduma za kupima Ukimwi kwa wachumba, pamoja na kusaidia mtu kujulisha mchumba wake kama amegundua kuwa ana Ukimwi, shirika likisisitiza hasa kupimwa kwa wachumba wa wagonjwa wa Ukimwi kwenye mazingira ya kiafya yoyote yale. Shirika la Afya la Dunia pia lilitoa mapendekezo kwenye vipimo vya Ukimwi vinavyofanyika kwenye jamii, mkiwemo mapendekezo ya kutoa huduma za kufanyia vipimo vya Ukimwi nyumbani kwa jamaa za mgonjwa wa Ukimwi. Katika maeneo yote ya kazi za shrika la Afya la Dunia, baadhi ya nchi zina mipango ya sera za kuongoza kujulisha mchumba kuhusiana na vipimo vya Ukimwi. Kwa kutegemea uchunguzi uliofanyika mwaka wa 2016 wa sera za huduma za kupima Ukimwi zilizotangazwa, asilimia 54 (sera 67 kati ya 123) zinapendekeza huduma za mtu kujulisha mchumba wake akigunduliwa kuwa ana Ukimwi; ingawa, ni tu sera ishirini kati ya hizo ambazo zinabainisha wazi kuwa mkakati huo unatekelezwa hivi sasa. Hivi leo, nchi 67 zina sera zinazoongoza watu waliogunduliwa kuwa na Ukimwi kuwajulisha wachumba wao.




**Mikabala ya watu kujulisha wachumba kuwa wana Ukimwi kama inavyofafanuliwa kwenye sera 67 za kitaifa.**

**Anwani ya picha hii: https://www.ncbi.nlm.nih.gov/books/NBK401676/figure/ch3.f2/?report0**

Nchi za Uganda, Rwanda, Tanzania na Kenya zote zimeanza kutekeleza miongozo ya Shirika la Afya la Dunia ya watu kujulisha wachumba wao wakigunduliwa kuwa na Ukimwi kama njia mojawapo ya kuzuia usambazwaji wa Ukimwi kupitia kupimwa Ukimwi. Kwa mfano, katika mwaka 2015, nchi ya Kenya ilianza kutekeleza miongozo hii kama mkakati wa kudhibiti Ukimwi nchini Kenya. Nchini Uganda, utekelezaji wa miongozo hii hutokea hasa miongoni mwa wachumba wa kina-mama wajawazito. Nchini Rwanda, miongozo hii imezingatiwa kwenye Sera ya Kukinga na Kudhibiti Ukimwi na Magonjwa ya zinaa.

Mwongozo wa Mradi wa dharura wa Marekani wa kudhibiti Ukimwi (PEPFAR) kwa nchi zote zinazofadhiliwa chini ya mradi huu unazingatia upimaji Ukimwi kwa jamaa, kusaidia mtu kujulisha mchumba wake akigunduliwa kuwa na Ukimwi, au kufuatilia wahusika wa mgonjwa wa Ukimwi, mikakati hii yote ikizingatia mkabala uleule wa kuwatafuta watu ambao huenda wakawa walihusika na mgonjwa wa Ukimwi, ama kama watoto wake aliowazaa au watu alioshiriki ngono nao, na kuwasaidia waweze kupata huduma za kupimwa Ukimwi. Kinyume na utekelezaji wa mwongozo huu, mashiriki yanayotekeleza miongozo hiyo hayajazingatia kanuni hii ya pili, Mkakati wa kusaidia mtu kujulisha mchumba kuwa ana Ukimwi umetekelezwa vibaya; na isitoshe, kwa namna ya haraka sana. Wanawake na wasichana wenye Ukimwi wanalalamika kwamba wanalazimishwa kutoa taarifa za wachumba wao na hawaheshimiwi na maafisa wa afya. Hizo taarifa za wachumba wao zinatumiwa kufichua hali ya Ukimwi ya wachumba hao, Hali hii imesababaisha kutoaminiana baina ya maafisa wa afya na wasichana na wanawake wenye Ukimwi kwa sababu imekiuka haki zao za kujiamulia kushiriki, faragha, usiri na usalama.

Wanawake na wasichana wenye Ukimwi wamekumbana na uhasama kutokana na vile mkakati wa kusaidiwa kujulisha wachumba hali ya Ukimwi umetekelezwa vibaya. Nchini Kenya, mwanzoni wa mwaka 2019, matukio matatu yaliripotiwa katika habari kuhusu wasichana wenye Ukimwi waliouawa kwa sababu wachumba zao walipata habari kutoka kwingineko na sio kutoka kwa wachumba zao wenyewe kwamba walikuwa na Ukimwi. Vilevile, nchini Burundi, mnamo mwaka 2019, msichana aliyekuwa na Ukimwi iliripotiwa kuwa aliuawa na mchumba wake, na mwingine alilazimika kutoroka na kujificha asije akapata madhara. Matukio mengine mengi kuhusu wanawake na wasichana wanaokumbana na uhasama kutoka kwa wachumba wao hayakuripotiwa na vyombo vya habari Kanuni za mradi wa PEPFAR[2] za mwaka 2020 hutaja kwamba upimaji wa haraka wa mchumba au mhusika wa mgonjwa wa Ukimwi ukomeshwe miongoni mwa makahaba, mashogi au kundi maalumu la watu lolote kwa sababu malalamiko yameibuka kuhusu vipimo vinavyofadhiliwa na mradi wa dharura wa PEPFAR kuwa vinatendeka kwa njia isiyozingatia umuhimu wa usiri, idhini ya mhusika na kuheshimu kikamilifu haki za wagonjwa. Hata hivyo, hali hii haizingatii wanawake na wasichana wanaoishi na Ukimwi kama kundi maalum la watu kwenye kanuni hizi ingawa wao ni waathiriwa wa shida hii

2 PEPFAR 2020 Country Operational Plan Guidance for all PEPFAR Countries

# Udhaifu katika Sera

**Mazingira ya kiuchumi-jamii ya Kiafrika:** Mikabala wa kusaidiwa kujulisha mchumba kuwa una Ukimwi inayopendekezwa na Shirika la Afya la Dunia inategemea uzoefu wa muda mrefu katika mazingira ya Marekani na Ulaya ambako hiyo mikabala imefaulu, pamoja na njia rahisi ya kufuatilia wahusika wa mgonjwa wa Ukimwi na kuwaelekeza kupata matibabu. Kabla ya kuanzisha mipango kama hiyo katika eneo la kusini ya Sahara barani Afrika, ni muhimu kutathmini kwanza mkabala huo kwa kuzingatia mazingira ya kiAfrika ya vijijini na mijini, ambayo yana hitilafu katika idadi ya watu wenye Ukimwi, makundi ya watu wanaoathirika hasa, na utamaduni, na mfumo wa hospitali usio imara na kipato haba. Ukimwi ni tofauti na ugonjwa wa kifua kikuu (TB) ambao utekelezaji wa mkakati wa kusaidia mtu kujulisha mchumba hufaulu, kwani Ukimwi ni Ugonjwa wa kipekee kuhusiana na namna wagonjwa wanavyobaguliwa katika jamii na jinsi hasi ambayo watu hufikilia wagonjwa wa Ukimwi. Utafiti zaidi unatakiwa kufanywa kuhusu kiasi cha faulu cha mkakati huu hasa katika maswala ya kukinga watu dhidi ya vitendo vya uhasama baada ya kujulisha wachumba zao kuwa wana Ukimwi.

**Ulinzi wa sheria kwa wachumba wenye Ukimwi:** Kwa jumla, miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki, hakuna sera thabiti ya mkakati wa kusaidiwa kujulisha mchumba kwamba uan Ukimwi, na miongoni mwa zile sera zilizopo, hakuna hata moja inayotaja sheria ya kuwalinda wagonjwa wa Ukimwi dhidi ya kupata madhara baada ya wao kujulisha wachumba zao kuwa wana Ukimwi. Nchi 19 hazitaji kwamba mgonjwa atoe idhini kwanza kabla ya kupimwa Ukimwi katika sera zake, na nchi 21 mkiwemo zile za ukanda wa Mashariki ya Afrika, kwa kiasi fulani, zina sera inayolazimisha mtu kujulisha mchumba akigunduliwa kuwa na Ukimwi. Shirika la Afya la Dunia haliungi mkono kitendo cha kulazimisha mtu kujulisha mchumba kwamba ana Ukimwi.

**Kudadisi na kufuatilia vitendo vya uhasama kutoka kwa mchumba:** Kutokana na malakamiko kwamba mkakati wa kusaidiwa mtu kujulisha mchumba kuwa ana Ukimwi unaweza kusababisha vitendo vya uhasama kutoka kwa mchumba dhidi ya mpenzi wake aliyepimwa kwanza (mgonjwa wa Ukimwi), sera zinazohusu mkakati huu zinafaa kueleza kikamilifu kuhusu namna ulinzi wa wagonjwa wa Ukimwi dhidi ya uhasama utakavyotekelezwa na kuzingatiwa ndani ya sera hiyo.

**Hitimisho:** Hapana shaka kwamba mkakati wa kusaidiwa kujulisha mchumba kuwa una Ukimwi umewasaidia wale wanaohitaji kupimwa Ukimwi na hurahisisha sana kukusanya watu kwa madhumuni ya kuteleleza malengo ya 90-90-90. Lakini, sera zilizo nyingi hazizingatii madhara ya kijamii yanayosababishwa na mkakati huo, hasa barani Afrika ambako wanawake na wasichana huchukua hadhi ya chini katika jamii. Sera hizo zinatakiwa kuimarishwa ili ziweze kulinda watu walio wa kwanza kupimwa Ukimwi na kisha wakatoa taarifa za wachumba zao. Mfumo wa sera hizi unatakiwa kuzingatia vizuizi vya msingi vya upimaji na kutoa matibabu kwa wagonjwa, ambavyo vinakiuka uwezo wa mgonjwa au mwuguzi, kwa mfano, mazingira ya kisheria/kisera, upatikanaji wa vifaa, kupata huduma, kuwepo kwa wafanyakazi, ukosefu wa kiunzi bora kati ya kupimwa na kupata matibabu, na vizuizi vingine vinavyohusiana na utoaji huduma bora. Kuna haja ya kupanua uvumbuzi kwa kuharakisha ukubalifu na upanuaji wa mikabala kifani ili kuboresha ufuatilizi wa wagonjwa wapya pamoja na vifaa vya kupimia na mbinu nyinginezo ya kufanyia vipimo. Isitoshe, kuzidisha mikakati inayofaulu kwa kupanua utumiaji wa mikabala iliyokwisha faulu kwingineko na kukuza vifaa, zana na mikabala mipya vinavyoungwa mkono na ushahidi ili kuzidisha matokeo badala ya kutumia mikabala ya kulazimisha pia ni muhimu.

# Mapendekezo kwa watungaji sera

- Wagonjwa wa Ukimwi wanatakiwa kupewa hiari mbalimbali ya mkakati wa kujulisha wachumba wao kuwa wana Ukimwi kama vile rufaa ya kimkataba, rufaa ya afisa wa afya au rufaa ya ubia; mkabala utakaochaguliwa utegemee hiari la mgonjwa.
- Huduma za kujulisha mchumba hali ya Ukimwi ziwe za kujitolea. Mikabala ya kulazimisha wagonjwa kujulisha wachumba zao kamwe yasikubalike. Watu wapewe ushauri kuhusu faida na hatari zilizopo ili waweze kutoa uamuzi wenye usalama na ujuzi.
- Idara za mahakama, polisi au watoa-huduma zisizo za kimatibabu zisihusike kwenye mipango ya watu kujulisha wachumba wao kuwa wana Ukimwi, hasa pale ambapo vitendo vya kundi fulani la watu vinachukuliwa kuwa vinavunja sheria.
- Sera za kusaidiwa kujulisha mchumba kuwa una Ukimwi zitaje njia za kulinda wagonjwa wa Ukimwi dhidi ya dhuluma baada ya wao kutangaza kuwa wana Ukimwi na kuwajulisha pia wachumba zao.
- Mradi maalumu wa marekani wa kudhibiti usambazwaji wa Ukimwi (PEPFAR) unatakiwa kusitisha utekelezaji wa mkakati wa utangazaji hali ya Ukimwi kwa mchumba kwa wanawake na wasichana wenye Ukimwi kama walivyofanya kwa makundi maalum ya watu mkiwemo washogi na makahaba hadi utakapotoa mwongozo kuhusu viwango tarajiwa na michakato ya kuhakikisha kwamba hospitali husika ina uwezo wa kuzingatia huduma za kupima zenye faragha, kujitolea kushiriki na kutoa idhini.
- Miradi yote inayoendeleza kutekeleza vipimo vya mchumba mmoja kwanza izingatie mkabala unaotanguliza maslahi ya mgonjwa, ambao unataja wazi kwamba mchumba anayepimwa kwanza asilazimishwe kutaja majina ya wachumba wake wa kingono, na pia uwe na njia za kutathmini kiasi cha faida na cha hatari ili kuamua kama faida zinazidi hatari katika harakati za kufuatilia wahusika wa mgonjwa huyu.
- Sera chanya zina umuhimu katika miradi inayofaulu na iliyo salama ya kusaidia mtu kujulisha mchumba wake kuwa ana Ukimwi. Nchi zinafaa kudadisi sera na sheria zake ili ziweze kuzingatia namna zinavyoweza kuwasaidia watu wenye Ukimwi. Kwa mfano, zinafaa kugeuza vitendo vya kulazimisha mtu kumjulisha mchumba wake akiwa na Ukimwi ambavyo vinaweza kusababisha ubaguzi; na kuunda mkakati wa kufuatilia uwezekano wa uhasama dhidi ya mchumba, kubagua au kuhukumu kisheria watu kutoka makundi maalumu na watu wenye Ukimwi; na kutobagua kwa misingi ya jinsia, sanasana kwa wanawake ambao ndio wengi zaidi miongoni mwa wagonjwa wa Ukimwi.
- Sheria na sera zinazobagua, kuhukumu au kunyanyasa makundi maalumu au wagonjwa wa Ukimwi zinatakiwa kuondolewa na kugeuzwa ili kuunda mazingira bora ya wanawake na wasichana kupata huduma za matibabau ya Ukimwi bila ya kuhofu kubaguliwa na/au kuhukumiwa.

## FOR MORE INFORMATION

The International Community of Women Living with HIV Eastern Africa (ICWEA)
Plot 1106, Ssenge - Kawanda Road,
Off Kayunga Kampala - Hoima Road,
P.O. Box 32252, Kampala, Uganda
Tel. +256 414531913 Mobile: +256392947313
Email: admin@icwea.org Twitter: @ICWEastAfrica
Facebook: ICW Eastern Africa
Website: www.icwea.org

AWDF AFRICAN WOMEN'S DEVELOPMENT FUND